OFISI YA RAIS - TAMISEMI
HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA

Simu: 0222184725
Email: bwmhs98@gmail.com
Website : www.benjamin.sc.tz

Benjamin W. Mkapa High School,
S. L. P. 15209,
DAR ES SALAAM.

Kumbukumbu Namba BWMHS/ GC/VOL. Tarehe: _____

Mwanafunzi : _____

YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO MWAKA - 2021/2022

Nafurahi kukuarifu rasmi ya kuwa umechaguliwa kujiunga na Shule hii ya **Benjamin William Mkapa High School** kidato cha **Tano** kwa mwaka wa masomo **2021/2022**, unatakiwa uripoti Shuleni tarehe _____ kwa ajili ya kuanza masomo rasmi.

Lipia ada na michango mingine katika Accounti ya Shule **NMB – ILALA** Na:- **20301100118** jina la Akaunti ni **Benjamin William Mkapa High School.** Wasilisha vifaa katika ofisi ya **Boharia** wa Shule.

Pamoja na taarifa hii napenda kukujulisha kuwa malipo yote yalipwe Banki kama ilivyoainishwa kwenye jedwali bila kupungua, **Original Bank Pay Slip** iletwe kwa **Mhasibu** ikiwa na jina la mwanafunzi, kidato chake na ikionesha **Tahsusi (combination)** aliyochaguliwa.

(a) FEDHA:

S/N.	AINA YA MALIPO	KIASI TSH.
1.	Karo ya Shule ya mwaka	20,000/=
2.	Taaluma	20,000/=
3.	Mock	20,000/=
4.	Tahadhari	5,000/=
5.	Ulinzi na vibarua wengine	30,000/=
6.	Nembo ya Shule 2	4,000/=
7.	Kitambulisho na Picha	6,000/=
8.	Ukarabati wa samani	15,000/=
9.	Afya	5,000/=
	JUMLA	**TZ SH.125,000/=**

VIFAA KWA MATUMIZI BINAFSI:

1. Jozi **2** za viatu vyeusi vipya vyenye kamba na visigino vifupi.
2. Jozi **4** za soksi nyeupe mpya kwa wasichana na wavulana soksi nyeusi.
3. School Bag – **1**
4. Scientific Calculator (Science)
5. English Dictionary (Arts)
6. T. Shirt (Blue)
7. Raba nyeupe

VIFAA KWA MATUMIZI YA SHULE:-

1. Lete Karatasi za Photocopy **A4 Bunda 2** aina moja wapo kati ya hizi zifuatazo:- **Dolphine** (cover yake rangi ya blue) **TOP COPIE** (cover yake rangi ya kijani).
2. Ruled paper 2 reams.
3. **PCB/PCM/PGM/EGM/ECA** alete vifaa (i) hapo chini
   (i) Street Broom (chelewa ya kusimama) 1
   (ii) Bahasha A3 **(12 Pcs)**

   HGE Counter Book **(3 Q) – 2, Soft Broom 2**

   HGK, HGL: Hard Broom **1, Spring file 12 PCS**

   HKL: Squezer **2, Ndoo 1 kubwa, toilet brush 2**

4. Unapaswa kuja na fomu zilizoambatanishwa na barua hii zikiwa zimejazwa kikamilifu. Fomu hizi ni viambatanisho **A, B & C.** Pamoja na Cheti cha **kuzaliwa, Leaving Certificate** ya Kidato cha **IV** na **Result Slip** (kila cheti kiwe Original na Photocopy yake.

5. **NB:** Matumizi ya **Simu** shuleni hayaruhusiwi ukikamatwa na simu darasani hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi yako.

Nakutakia heri na mafanikio ukiwa katika Shule hii.

Ni matumaini yangu kuwa daima utatii taratibu na Kanuni za Shule.

KARIBU SANA

JOSEPH L. DEO
MKUU WA SHULE

KIAMBATANISHO 'A'

HALMASHAURI YA MANISPAA YA ILALA
BENJAMIN WILLIAM MKAPA HIGH SCHOOL

FOMU YA KUANDIKISHWA

Picha mwanafunzi

(a) **Ijazwe na mwanafunzi**:

1. Jina kamili la mwanafunzi _____
2. Uraia _____
3. Dini _____
4. Tarehe ya kuzaliwa _____
5. Mkoa aliozaliwa _____
6. Yatima/Siyo yatima_____
7. Kata unayoishi_____
8. Umbali kati ya unapoishi na Shule ilipo km 3 ☐ zaidi ya km 3 ☐
9. Shule alizosoma kabla ya kuja Sekondari ya Benjamin William Mkapa

JINA LILILOANDIKISHWA SHULENI	SHULE YA MSINGI/ SEKONDARI	TAREHE NA MWAKA ALIOANZIA	TAREHE NA MWAKA ALIOTOKA
1.	1.	1.	1.
2.	2.	2.	2.
3.	3.	3.	3.
4.	4.	4.	4.

(b) **Maelezo binafsi ya mzazi / mlezi**

Picha mzazi/mlezi

Jina kamili la Mzazi / Mlezi _____

1. Uraia _____
2. Anuani kamili mjini DSM _____
3. Sehemu unayoishi _____
4. Mtaa _____
5. Namba ya nyumba _____
6. Namba ya simu _____(ya haraka)
7. Jina la Mwajiri na Idara _____
   - Anuani : _____
   - Namba ya simu : _____
   - Kazi ya mzazi / mlezi : _____

   (Mfano : Karani, Meneja, Mwalimu n.k.

   Sahihi ya mzazi / mlezi _ _____

KIAMBATANISHO 'B'

Mkuu wa Shule,
Benjamin William Mkapa High School,
S.L.P. 15209,
DAR ES SALAAM.

Picha ya Mzazi / Mlezi

YAH: AHADI YA MZAZI / MLEZI KUKIRI KUKUBALIANA NA SHERIA, KANUNI NA MAELEKEZO YA SHULE

Mimi _____ Mzazi / Mlezi wa mwanafunzi_____ wa kidato cha **Tano** katika Shule ya Sekondari ya Benjamin William Mkapa, nathibitisha kuwa nakiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo yote ya shule. Naahidi pia kumsimamia mwanafunzi afuate sheria, kanuni na taratibu za shule. Naahidi pia kutoa ushirikiano na shule kwa manufaa ya mwanangu na kulipa ada na michango kwa wakati.

Jina la Mzazi / Mlezi : _____

Sahihi ya Mzazi / Mlezi : _____

Namba ya simu: _____

KIAMBATANISHO 'C'

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
PRIME MINISTER OFFICE – TAMISEMI
ILALA MUNICIPAL COUNCIL
STUDENT MEDICAL CERTIFICATE

To be completed by a Government Medical Officer and returned to be Headmaster of Benjamin William Mkapa High School, P. O. Box 15209, DSM.

To the Medical Officer, Date: _____

_____
_____
_____

RE: _____

Please, examine the student mentioned above and comment on his / her health by responding to the following items. Kindly put a tick or cross in from of either **YES** or **NO** as you find appropriate.

JOSEPH L. DEO
HEDMASTER

3. Does the student have problems in connection with:

   (a) Sight? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state _____

   (b) Hearing? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state _____

   (c) Speech? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state _____

   (d) T.B? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state _____

   (e) Blood pressure? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes, state _____

   (f) Any physical disability? **(1) No** **(2) Yes**
   If yes state _____

4. Do you, therefore, recommend the said student medically fit for studentship at this School **(1) No (2) Yes. If no, please state reasons**.
   _____

   Date: _____ **Name & Signature of M. O** _____

   Designation & stamp

OFISI YA RAIS TAMISEMI
HALMASHAURI YA JIJI LA DAR ES SALAAM

BENJAMIN WILLIAM MKAPA HIGH SCHOOL

Shule ipo kwa ajili ya kutoa Elimu kwa wanafunzi. Kama ilivyo katika jamii yoyote yenye lengo maalumu ni lazima shule iwe na sheria au taratibu zitakazowezesha jamii ya Shule kutekeleza majukumu yake. Sheria na taratibu hizo ni lazima ziwekwe wazi na zieleweke na kila mmoja na zifuatwe kikamilifu.

Zifuatazo ni kanuni au taratibu zinazohusu wanafunzi wa shule hii zenye lengo la kuweka mazingira ya ufanisi katika kazi na malezi hapa shuleni kulingana na matakwa ya Taifa letu la Tanzania.

1. **MIPAKA YA SHULE:**
Ni wajibu wa kila mwanafunzi kujua eneo la shule. Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea maeneo yafuatayo wakati wa muda wa masomo darasani.

(a) Chumba cha walimu (Staff room) na vyumba vingine vya idara mbalimbali.
(b) Maabara ya Sayansi (isipokuwa wakati wa kipindi husika).
(c) Ofisi ya Utawala na ghala zote
(d) Ni marufuku kwenda maeneo ya vibanda vilivyozunguka shule.
(e) Maeneo ya miradi
(f) Nyumba za walimu
(g) Maeneo ya shule jirani

Kukutwa kwenye maeneo yaliyotajwa wakati wa masomo darasani ni kukiuka sheria za shule. Mwanafunzi ataandhibiwa. Hivyo basi mwanafunzi anapaswa kubaki darasani muda wote wa vipindi hadi kengele ya kutoka inapogongwa.

2. **RUHUSA YA KUTOKA NJE YA MIPAKA YA SHULE AU NJE YA MKOA WA DAR ES SALAAM.**
Ruhusa ya kutoka nje ya shule kwa muda fulani tu itatolewa na mwalimu wa zamu kwa kutoa kibali. Kwa ruhusa za kutoka nje ya Mkoa wa Dar es Salaam, mwanafunzi lazima apate kibali cha Mkuu wa Shule.

3. **MATIBABU :-**
(a) Matibabu yote ya awali yatafanyika katika Zahanati ya Shule.

(b) Inapobidi kwenda nje ya shule kwa ajili ya matibabu ni lazima mwanafunzi apate kibali cha Nurse wa shule na mwalimu wa zamu/Makamu Mkuu wa Shule.

(c) Shule haitawajibika kurudisha gharama zilizotumika kumtibu mwanafunzi katika Zahanati/Hospitali ya binafsi/Serikali.

4. **LUGHA YA MAWASILIANO :-**
Lugha rasmi ya mawasiliano hapa shuleni ni Kiingereza. Hivyo tumia kiingereza wakati wote isipokuwa wakati wa kipindi cha Kiswahili.

5. **HESHIMA/MWENENDO MZURI AMBAO MWANAFUNZI ANAPASWA KUUFUATA AWAPO SHULENI.**

(i) Kusimama na kumsalimia mtu yoyote anayemzidi umri anapoitwa, anapoingia darasani au kwenye mkusanyiko/mkutano.

(ii) Kutumia Lugha nzuri wakati wote kati yao wenyewe, kwa walimu na watu wengine.

(iii) Kuheshimu Bendera ya Taifa, picha za viongozi wa Serikali nembo ya Taifa "Coat of Arms" na wimbo wa Taifa.

(iv) Kuheshimu ofisi za Shule, mali binafsi na mali ya umma.

(v) Kutovuta sigara, kutofuga ndevu na kucha na hutakiwi kuwa na nywele ndefu .

(vi) Kuvaa sare inayojulikana kwa wanafunzi na jumuiya nzima na iwe katika mshono unao kubalika na kulingana na heshima inayosisitizwa kitaifa.

(vii) Kuwepo ndani ya eneo la shule (sehemu) husika kwa muda wote wa masomo.

(viii) Kufika shuleni siku zisizokuwa za masomo kwa kibali au ruhusa maalum.

(ix) Mwanafunzi haruhusiwi kuchangia mchango wowote ule bila ya kibali.

(x) Mwanafunzi haruhusiwi kuruka uzio/ukuta wa shule.

(xi) Mwanafunzi haruhusiwi kuwa nyuma ya jengo jipya (Bakhresa) kwa muda wowote ule.

(xii) Hairuhusiwi wanafunzi kuwepo eneo la shule baada ya masomo kwisha yaani saa 12.00 jioni isipokuwa kwa shughuli maalum iliyopata kibali cha Uongozi wa Shule.

(xiii) Mwanafunzi anapaswa atoe taarifa kwa tukio lolote la uhalifu kwa Uongozi wa Shule/walimu wa zamu.

(xiv) Mwanafunzi anapaswa kufanya mitihani yote bila kukosa isipokuwa kwa taarifa maalum.

(xv) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria masomo rekebishi "remedia classes" yanayotolewa shuleni "remedial classes" muda wowote baada ya masomo siku za kawaida au wakati wa likizo.

(xvi) Mwanafunzi anapaswa kuwahi shule au sehemu yeyote atakapohitajika mfano kwenye sherehe za muungano n.k.

(xvii) Mwanafunzi anapaswa kuyapenda masomo yote anayofundishwa/kusoma mchepuo wake mfano kidato cha I na II masomo yote wanapaswa wayapende na kuyasoma kwa bidii. Kidato cha V na VI masomo ya ziada General Studies na BAM yanapaswa kusomwa sawa na masomo ya Combinations mfano HKL, PCM, PCB n.k.

(xviii) Mwanafunzi atawajibika kufanya usafi na kutunza mazingira na mali za shule sehemu zote atakazopangiwa.

(xix) Kufika kwa haraka eneo husika wakati wa kengele ya dharura.

(xx) Mwanafunzi anapaswa kuhudhuria vipindi vya dini bila kukosa na kwa wakati.

(xxi) Mwanafunzi haruhusiwi kugombana na mwanafunzi mwenzake, mwalimu au mtu yoyote yule.

(xxii) Mwanafunzi haruhusiwi kuandika maandishi pasipotakiwa mfano ukutani, vitabuni n.k.

(xxiii) Mwanafunzi haruhusiwi kuju na simu wala kutumia katika maeneo ya shule.

(xxiv) Mwanafunzi haruhusiwi kuhubiri dini awapo shuleni isipokuwa kwenye kipindi cha dini.

(xxv) Mwanafunzi anapaswa kukubali uteuzi wowote ule mfano kushiriki katika michezo, maandamano yaliyorasmi n.k.

(xxvi) Mwanafunzi haruhusiwi kutoa/kubandika tangazo bila kibali.

(xxvii) Mwanafunzi haruhusiwi kufanya biashara shuleni.

(xxviii) Mwanafunzi hapaswi kwenda kwenye maeneo ya baa kumbi za starehe akiwa na sare za shule/nguo za nyumbani.

(xxix) Mwanafunzi haruhusiwi kuja na silaha wala kutumia silaha awapo shuleni.

5.0 **MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULENI KWA MWANAFUNZI:**

1. Wizi
2. Uasherati
3. Ulevi na madawa ya kulevya
4. Uvutaji bangi
5. Makosa ya jinai
6. Kupigana au kupiga mwanafunzi/mwalimu
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
8. Kudharau Bendera ya Taifa
9. Kuoa au kuolewa
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule
11. Kutoa mimba
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu.
13. Kukataa adhabu kwa makusudi
14. Utoro uliokithiri

6.0 **ADHABU :**

(i) Adhabu zinaweza kutolewa na mwalimu yeyote kwa mwanafunzi aliyeonesha utovu wa nidhamu.

(ii) Kosa linapokuwa kubwa litaandikwa katika jalada la mwanafunzi katika kitabu cha kumbukumbu za adhabu.

(iii) Adhabu zitatolewa kulingana na uzito wa kosa.
Sheria na kanuni hizi zimeidhinishwa na Bodi ya Shule.

JOSEPH DEO
MKUU WA SHULE